KUWASILISHA MALALAMIKO YA KUBAGULIWA KATIKA MAKAZI

JINSI YA KUWASILISHA:

Ikiwa unaamini kwamba umebaguliwa katika suala la makazi, unaweza kuwasilisha malalamiko kwa Tume ya Haki za Binadamu ya Jiji la Iowa.

LINI KUWASILISHA:

Ni sharti uwasilishe malalamiko ndani ya siku 300 tangu kutokea kwa tukio la ubaguzi.

MAHALI PA KUWASILISHA:

Unaweza kuwasilisha malalamiko katika ofisi ifuatayo:

Tuma ya Haki za Binadamu
ya Jijini la Iowa
City Hall
410 E. Washington Street
Iowa City, IA 52240
(319) 356-5022; (319) 356-5015
(319) 356-5014

KIPEPESI: (319) 887-6213

humanrights@iowa-city.org
www.icgov.org/humanrights

EQUAL HOUSING OPPORTUNITY

3/16

SHERIA YA HAKI YA MAKAO JIJINI IOWA

Tume ya Haki za Binadamu
410 E. Washington St.
Iowa City, IA 52240
www.icgov.org/humanrights
humanrights@iowa-city.org

Jiji la JIJI LA IOWA

©2016

UBAGUZI KATIKA MAKAO

Kanuni ya Manispaa ya Jiji la Iowa, Mada ya 2, Kanuni ya Haki za Binadamu, inapiga marufuku ubaguzi katika huduma za makao kwa misingi ya **UMRI, RANGI, IMANI, ULEMAVU, UTAMBULISHO WA JINSIA, HALIYA NDOA, HALIYA FAMILIA, NCHIYA ASILI, KABILA, DINI, JINSIA, MWELEKEO WA JINSIA, KUWA AU KUTOKUWA NA WANAOKUTEGEMEA AU KUSAIDIWA NA SERIKALI KULIPA KODI** (hii unajumuisha Ruzuku ya Vocha ya Nyumba pamoja na ruzuku nyingine za kodi zinazofanana na hiyo [1]). Ubaguzi wowote unaotokana na **SABABU YOYOTE KATIYA HIZI** hairuhusiwi katika vipengele vifuatavyo vya huduma za makazi.

1. KUKATAA KUONYESHA, KUKODISHA, KUPANGISHA, KUUZA AU KUBADILISHANA NYUMBA AU MAKAO YA AINA YOYOTE

Makazi ni nyumba, jengo au sehemu ambapo mtu anaweza kukaa au iliyoundwa au inayonuiwa kutumiwa kwa ajili ya kuishi, mtu mmoja, watu au familia na ardhi tupu inayouzwa au kukodishwa kwa lengo la kujengea au kuwekewa jengo au sehemu ya ujenzi. Nyumba za fleti, ghorofa, nyumba za kuishi familia mbili na majengo mengine kama hayo, nyumba zinazohamishika, trela nyumba na nyumba za binafsi zimejumuishwa katika fasili hii.

Kwa sababu ya ulinzi ulio nao:
Je, umewahi kukatazwa kuangalia nyumba au makazi au kunyimwa fursa ya kukodisha au kununua nyumba ambayo wengine wanaruhusiwa?

Je, uliambiwa nyumba imechukuliwa, ilihali bado kulikuwa na kibao cha "inakodishwa" au "inauzwa" siku iliyofuata?

Je, jibu ulilopokea kwenye simu lilikuwa tofauti na ulilopewa ana kwa ana?

Je, kulikuwa na orodha ya wanaosubiri? (Huu si ubaguzi moja kwa moja, bali ni jambo linalofaa kufuatiliwa.)

2. KUSABABISHA VIGEZO, MASHARTI AU FURSA ZISIZO SAWA KATIKA KUPATA MAKAO

Kwa sababu ya ulinzi ulio nao:
Je, umenyimwa fursa nyingine ambazo wengine wanapata kama vile ukarabati na huduma , au kutumia bwawa au jumba la mazoezi la unapokaa, iwe ulikuwa mkazi au mgeni?

Kama ulipewa ilani ya kuhama, ulitendewa tofauti na wapangaji wengine?

Je, ulipewa bei ya kukodi au ya kununua iliyo juu zaidi ya bei iliyotangazwa? Je, ulitakiwa ulipe amana ya juu zaidi?

3. KUSABABISHA VIGEZO, MASHARTI NA FURSA TOFAUTI KWA AJILI YA MIAMALA YOYOTE YA NYUMBA, IKIWEMO MSAADA WA KIFEDHA KWA UNUNUZI, UJENZI AU UKARABATI WA NYUMBA

Kwa sababu ya ulinzi ulio nao:
Je, ulifanyiwa uchunguzi wa ziada wa kufaa mkopo au kutakiwa kuwa na mdhamini wa ziada tofauti na wengine? Je, mkopeshaji au dalali alikataa kujumuisha mapato ya mwenzi wako wa ndoa kwenye ombi lako la deni au upangaji? Au walitaka kujumuisha mapato hayo kinyume cha matakwa yako?

Je, ulitakiwa kuweka dhamana kubwa au kuwekewa riba ya juu ikilinganishwa na wanunuzi wengine?

Je, umekatazwa mkopo wa nyumba au ukodishaji wa nyumba?

Je, uliulizwa kama unanuia kuanzisha familia?

4. KUSAMBARATISHA NA/UA KUTENGANISHA JAMII

Kwa sababu ya ulinzi ulio nao:
Je, ulikatazwa waziwazi kutafuta nyumba katika mitaa fulani?

Je, dalali wa ukodishaji au uuzaji alikuonyesha sehemu au eneo moja pekee ingawa ulitaka kuona maeneo mengine?

5. KUJUMUISHA AU KUFUATA MAKUBALIANO AMBAYO NI YA KIBAGUZI

6. KUTANGAZA UBAGUZI AU MAPENDELEO KATIKA MAKAO; KUTANGAZA MOJA KWA MOJA AU KWA NJIA FICHE KWAMBA MTU WA IANA FULANI HATAKIWI AU HARUHUSIWI

Kuuliza au kutaja hoja zenye ubaguzi. Mfano: "Watu wa Sehemu ya 8 Hawaruhusiwi!"

Kwa sababu ya ulinzi ulio nao:
Je, mwenye nyumba, msimamizi, mkopeshaji au dalali alikuuliza au kutaja makundi yanayolindwa ambayo yametajwa hapa juu, alipozungumza nawe?

7. KUSAIDIA NA KUKINGA VITENDO VISIVYO VYA HAKI VINAVYOHUSU MAKAO

Kumzuia mtu yeyote kufuata desturi halali za kupata makao au kumsaidia mtu kuvunja kanuni za kupata makao.

8. KULIPIZA KISASI DHIDI YA MFANYAKAZI AU DALALI ANAYEFUATA KANUNI SAHIHI ZA MAKAZI KWA VITENDO KAMA VILE KUMBOMOLEA, KUMFUTA KAZI AU KUMPA MALIPO YASIYOSTAHIKI

9. KUKATAA KUPOKEA NA/AU KUWASILISHA KIBALI CHOCHOTE CHA KUNUNUA, KUKODI, KUNUNUA AU KUPANGISHA NYUMBA

10. KUTISHIA WENYEJI, KUNYIMA MIKOPO, AU UFUKUZAJI

KUWATISHIA WENYEJI- kunaweza kutokea wakati madalali wa nyumba wanapohimiza uorodheshaji na uuzaji wa nyumba (na hivyo kujiundia biashara) kwa kutumia mbinu za kusababisha hofu kwa kuwaonya wenyeji kwamba watu wa rangi au kabila nyingine, kwa mfano, watahamia eneo hilo. Kauli kama vile 'watu wabaya wanahamia eneo hili, au kutaja kwamba 'viwango vya elimu vinashuka' au 'mtaa unabadilika' ni mifano ya mtindo huu.

KUNYIMA MIKOPO- ni pale ambapo wakopeshaji na mashirika ya bima yanapowanyima watu wa mitaa fulani huduma au kuwaongezea gharama, ada na/au kufanya riba zao kuwa za juu kwa sababu wapo miongoni mwa wanaopokea ruzuku.

UFUKUZAJI- ni tabia inayoweza kuathiri uamuzi wa mtu kuchagua anapoishi kutokana na tabaka au hali ya kulindwa. Mifano ni pamoja na kuwaelekeza watu katika mitaa ambapo watu wa jamii yako wanapoishi na kuchagua orodha za nyumba au kutomshauri kuhusu nafasi zilizopo kwa lengo la kubagua.

[1] Inaanza kutumika tarehe 1 Juni, 2016